msingi pia imekarabatiwa na kuongezwa madarasa, mabweni na matundu ya vyoo.

MWANANCHI UK 10.

# Wakopeshwa ng'ombe 350

Burhani Yakub, Mwananchi

**Tanga.** Changamoto ya uhaba wa maziwa ambao umekuwa ukikikabili kiwanda cha Tanga Fresh inataanza kupata ufumbuzi baada ya wafugaji kupewa mikopo ya ng'ombe 350 wa maziwa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) wenye thamani ya Sh900 milioni.

Ng'ombe hao wanatarajia kuongeza uwezo wa ukusanyaji wa maziwa kwa kiasi cha kuanzia lita 3,000 hadi 3,500 kwa siku moja.

Katibu Tawala Mkoa wa Tanga,Pili Mnyema alisema hayo jana alipozungumza na Mwananchi kuhusiana na mikakati kuongeza uzalishaji wa maziwa mkoani hapa.

Alisema mkoa umepunguza changamoto ya tasnia ya maziwa iliyokuwepo ikiwakabili wafugaji katika kipindi cha mwaka 2021/22 ya kudai malipo ya maziwa kutoka kiwanda cha Tanga Fresh Limited na sasa wanalipwa kwa wakati.

Alisema kiasi cha maziwa yanayochakatwa na Tanga Fresh kimeongezeka kutoka lita 11,000 kwa siku mwaka 2021/22 hadi kufikia lita 23,000 kwa siku Desemba mwaka jana.

"Katika kuhakikisha upatikanaji wa maziwa unaongezeka vimejengwa vituo vipya nane vya ukusanyaji maziwa katika Wilaya za Korogwe,Tanga jiji, Mkinga na kuwezesha mkoa wa Tanga kuwa na vituo 44 kutoka 36 vilivyokuwepo mwaka 2022 na hivyo kuwa na ongezeko la lita 10,000 kwa siku moja" alisema katibu tawala huyo.

Alisema mbali ya tasnia ya maziwa, Mkoa wa Tanga kwa sasa una jumla ya ng'ombe 1,004,793 ikilinganishwa na ng'ombe 975,444 waliokuwepo mwaka 2022 ambapo kati yao wa asili idadi yao in 904,609 na wa kisasa wapo 100,184.

"Mkoa kwa sasa una hekta 695,262 za eneo linalofaa kwa malisho yenye uwezo wa kuhimili ng'ombe 797,354 kati ya 1004,793 waliopo hivyo kuwa na ongezeko la ng'ombe 207,439 kulingana na uwezo uliopo" alisema.

John Semnkande, mfugaji wa ng'ombe wa maziwa na mwanachama wa Chama cha Wafugaji wa Wilaya ya Pangani alisema wafugaji wameonyesha kuwa na juhudi katika kuendeleza sekta hiyo, hiyo ipo haja kwa Serikali kuwawekea mipango yenye kuwainua zaidi kiuchumi.

# Walioathirika Hanang waomba wapewe mifugo

Janeth Mushi, Mwananchi
jmushi@mwanachi.co.tz



Baadhi ya wafugaji wakinywesha maji ng'ombe wilayani Hanang, mkoani Manyara kabla ya kutokea kwa maporomo ya mlima Hanang . Picha Maktaba.

**Hanang.** Baadhi ya wafugani wilayani Hanang mkoani Manyara, wameiomba Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo kuwasaidia mifugo michache ili waanze upya kazi ya ufugaji.

Walisema wengi wao walikuwa wakiendesha maisha yao kwa kutegemea kipato walichokuwa wakikipata kutoka na ufugaji ng'ombe, mbuzi na kuku.

Wakizungumza *Mwananchi* juzi, walisema maafa yaliyotokea Hanang Desemba 3,2023 yaliwaacha maskini kwa kuwa mifugo, nyumba na mashamba yao yaliharibiwa na tope lililowaachia simanzi katika maisha yao.

Magdalena Hanga, anayeishi Kitongoji cha Jorodom Kati alisema amepoteza mbuzi 20, kuku 15 na ng'ombe watano na sasa anaishi maisha magumu.

Alisema alimpoteza mume wake, watoto wake wawili na wajukuu wawili na mifugo aliyokuwa akitegema kwa kipato chake cha kila siku.

"Nimepoteza familia yangu, sina mbuzi, ng'ombe wala kuku, naomba Serikali itusaidie tuweze kuendelea na shughuli za ufugaji tulizokuwa tunategemea kujipatia kipato." alisema

"Nilikuwa nakamua maziwa ya ng'ombe na kuuza mayai ya kuku kwa ajili ya kupata matumizi ya watoto shule na mahitaji mengine ya familia, sasa sina mifugo na sijui maisha yangu yatakuwaje na hali ngumu iliyopo hivi sasa" alisema.

Mfugaji mwingine, Philipo Mayo ambaye ni mkazi wa Gendabi, alisema maafa hayo yamemsababishia hasara kubwa na hajui ni kwa namna gani atarejea katika hali ya kawaida.

Alisema nyumba aliyokuwa akiishi ilisombwa na maporomoko hayo na eneo lake la mgahawa liliharibiwa.

Alibainisha kuwa kuku 30 aliokuwa akiwafuga kwa ajili ya mayai nao walisombwa na maporomoko hayo ya matope.

"Siku ya tukio nilifanikiwa kutoka ndani ya nyumba salama mimi na mke wangu na watoto.Kuku 30 na mbuzi walisombwa ila mbuzi watano na kondoo wawili walifanikiwa kutoka kwenye tope upande mwingine wa matope, kuku wote walikufa na ndiyo nilikuwa nategemea kama chanzo cha kipato cha familia," alisema na kuongeza:

"Nilikuwa na biashara ya mgahawa huku nako nyumba yote ilibomoka na vyombo vyote viliondoka hili janga limenigusa sana tunashukuru Serikali imetusaidia upande wa chakula,mavazi na malazi ila tunaomba ituangalie kwa upande wa mifugo pia." alisema

Emanuel Darema mkazi wa Kitongoji cha Jorodom Kati, Kata ya Jorodom, alisema katika maafa hayo amepoteza ng'ombe watatu alikuwa akiwakamua na kuuza maziwa.

Alisema pia eneo alilokuwa ametenga kwa ajili ya malisho ya mifugo hiyo nalo limeharibiwa na maporomoko hayo.

Abainisha kuwa kutokana na kutegemea mifugo hiyo kama chanzo cha mapato, aliiomba Serikali na wadau iwasaidie wapate mifugo kwa kuwa walikuwa wakitegemea kwa ajili ya uchumi.

"Tulipata hasara kubwa inayotokana na janga hili ambapo watu wengi wamepoteza rasilimali nyingi na nilipata hasara kubwa. Nimepoteza ngombe watatu waliokuwa vyanzo vyangu vya uchumi nilivyovitegemea kwa ajili ya kulima na maziwa,"alisema

"Maisha kwa ujumla yamevurugika kwani sisi tunatumia maji ya bomba ambayo tulivuta kwa nguvu zetu wenyewe ila sasa hivi hamna tunaishi maisha ya shida kwa kutegemea maji tunayoletewa na serikali.

"Shamba liliharibiwa kama unavyoona kila mmoja alikuwa anategemea eneo lake kwa ajili ya kulisha mifugo pia kwa hiyo maeneo madogo na mifugo tumedidimia kwani mifugo imesombwa karibu yote," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Hanang,- James Gejaru, alisema licha ya takwimu za athari kwa mifugo kuendelea kukusanywa ni vema Serikali na wadau kuwasaidia mifugo.

"Wafugaji tumepata madhara kwa kupoteza tegemeo letu kwa masuala ya kiuchumi, tunaiomba Serikali na wadau wote watusaidie mifugo kwa kuwa tunategemea kuendesha maisha yetu ikiwemo kuwasomesha watoto kwa mifugo," alisema

Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janeth Mayanja, alisema katika maporomoko hayo kuna maeneo ambayo yameathirika ikiwemo wafugaji ambao mifugo yao ilizolewa na maji na tope lakini mifugo mingine iliyobaki ilikuwa na dalili ya kupata ugonjwa wa kimeta kwa hiyo Serikali imepeleka dawa kwa ajili ya mifugo iliyobaki ili iwe salama.

**ZAIDI**

**Serikali kusaidia ujenzi wa nyumba**

Rais Samia Suluhu Hassan, alipofanya ziara wilayani Hanang, Desemba 7, 2023 aliahidi kuwa wataalamu wa Serikali, wametenga eneo ambalo litatumika kuwahamisha waathirika wa maporomoko ya tope.

Alisema Serikali itawaunga mkono katika ujenzi wa makazi mapya ya kudumu.

**89**
Idadi ya watu waliopoteza maisha baada ya maporomoko ya mlima Hanang.

**139**
Watu waliojeruhiwa katika maporomoko hayo yaliyosababisha watu kukosa makazi na kupoteza mali.